

Muhtasari


- Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi mwa nchi na nyanda za juu kusini magharibi hususan katika kipindi cha mwanzo (siku tano za mwanzo) cha dekadhi.
- Ukanda wa kusini na pwani yote inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua kwa kipindi chote cha dekadhi.
- Hali ya mazao na malisho inatarajiwa kuimarika kutokana na kuimarika kwa unevunvevu kwenge udongo.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2018

Katika kipindi hicho, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika kidogo wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo. Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kubaki katika maeneo ya Tanzania. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani na kusababisha upepo kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine kumekuwapo na joto la bahari la chini kidogo ya wastani katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola)

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, maeneo mengi ya nchi pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua za chini ya wastani (chini ya 75% ya wastani wa mvua kwa siku kumi). Hata hivyo, mvua za juu ya wastani (zaidi ya 124% ya wastani wa mvua kwa siku kumi) zilinyesha katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora na Ruvuma kama inavyoonekana kwenye kielelezo.



Kielelezo. Kiasi cha mvua (%) kipindi cha tarehe 21-31, Machi 2018.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2018

Katika kipindi cha siku kumi, maeneo mengi ya nchi yalikuwa na upungufu wa mvua hali ambayo ilisaidia shughuli za palizi pamoja uwekaji wa dawa za kuulia wadudu waharibifu wa mazao. Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua mahindi yalikuwa katika hatua ya kutoa maua na kubeba hususan katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Dodoma, Singida, Tabora, Kigoma, Ruvuma na Mtwara. Wakulima katika maeneo haya wanajishughulisha na palizi. Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Mikoa ya Mara, Kagera and Manyara) wanaendelea na shughuli ya palizi ambapo mahindi yapo katika hatua ya jani la tatu na jani la tisa isipokuwa katika wilaya ya Babati na Mkoa wa Mwanza mazao yapo katika hatua yakutoa mbelewele. Hata hivyo, wadudu waharibifu aina ya viwavi jeshi wametaarifa kuwepo katika maeneo mengi ya mkoa wa Mara ambapo wilaya ya Serengeti ndiyo imeathirika zaidi kutokana na uharibifu wa mazao uliofanywa na wadudu hao.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2018

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, mabonde ya Wami, Ruvu, Ruvuma na Rukwa kutokana na mvua zinazoendele.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRIL 1-10, 2018

Katika kipindi hiki cha siku kumi (dekadi), migandamizo mikubwa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa

mvua (ITCZ) unatarajiwa kuanza kusogea taratibu kuelekea kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea upepo kuvuma kutoka mashariki na kusababisha upungufu wa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi hususan katika kipindi cha pili (siku tano za mwisho) cha dekadhi hii. Kwa ujumla, vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, magharibi mwa nchi na nyanda za juu kusini magharibi hususan katika kipindi cha mwanzo (siku tano za mwanzo) cha dekadhi hii wakati ukanda wa kusini na pwani yote inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua kwa kipindi chote cha dekadhi.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRIL 1-10, 2018

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara); magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Kuna tarajiwa kuwepo na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Kuna tarajiwa kuwepo na vipindi vya mvua katika maeneo machache

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Kuna tarajiwa kuwepo na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (Mikoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Kuna tarajiwa kuwepo na Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2018

Hali ya unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kuongezeka katika maeneo mengi ya mikoa ya kusini na pwani yote ya bahari ya Hindi. Pia baadhi ya sehemu ya ziwa Viktoria, ukanda wa magharibi, nyanda za juu kusini magharibi unyevunyevu kwenye udongo unatarajiwa kuongezeka kutokana na mvua zinazotarajiwa katika siku tano za mwanzo wa dekadhi. Vipindi vya hali ya ukavu vinatarajiwa kusaidia shughuli za palizi pamoja na unyunyiziaji wa dawa katika mazao kuzuia wadudu waharibifu. Hali ya maji pamoja na malisho vinatarajiwa kuimarika nchi nzima. Hivyo, wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRIL 1-10, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua zinazotarajiwa. Wananchi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uvunaji maji ya mvua na kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3 - Ubungo Plaza - Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam - Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 - 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 - 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz